# BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR

70 Barabara ya Chukwani,
Buyu
70490 Mjini Magharibi,
S. L. P 902 Chukwani,

Simu: +255 24 224 2000
Nukushi: +255 24 224 2000
info@zanzibarassembly.go.tz

## MUHTASARI WA RIPOTI YA KAMATI YA MAWASILINO, ARDHI NA NISHATI YA BARAZA LA WAWAKILISHI KWA MWAKA WA FEDHA 2023/2024

***Mheshimiwa Spika,*** Naomba uniruhusu nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu, mwingi wa rehma, kwa kutujaalia uzima na kutuwezesha kukutana tena katika Mkutano huu wa Kumi na Nne, Mkutano ambao shughuli yake kuu ni kujadili Ripoti za Kamati za Kudumu kwa Baraza hili la Kumi la Wawakilishi Zanzibar.

***Pia,*** nachukua fursa hii kukupongeza wewe binafsi pamoja na wasaidizi wako kwa jinsi mnavyokiongoza na kukiendesha chombo hiki, tunamuomba Mwenyezi Mungu akuzidishieni hekima na busara katika kutekeleza majukumu yenu.

***Mheshimiwa Spika***, Kadhalika, nawashukuru sana Waheshimiwa Wajumbe wa Kamati ya Mawasiliano, Ardhi na Nishati kwa kuendelea kuniamini na kunipa imani ya kuwaongoza na kunipa mashirikiano makubwa, jambo

ambalo limenipa nguvu na pia limesaidia kufanikisha vizuri majukumu ya Kamati yetu. Kwa hakika weledi na umahiri wao umesaidia kwa kiasi kikubwa sana kupatikana kwa ripoti hii hadi leo hii tunaiwasilisha.

***Mheshimiwa Spika,*** Kamati ya Mawasiliano, Ardhi na Nishati, ni miongoni mwa Kamati za Kudumu za Baraza la Wawakilishi iliyoundwa kwa mujibu wa Kanuni ya 107 ya Kanuni za Baraza la Wawakilishi, Toleo la mwaka 2020 na majukumu yake ni kama yale yaliyokwisha kuelezwa katika jadweli la Kwanza. Kamati hii inafanyakazi na Wizara tatu zifuatazo: -

(1) Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi

(2) Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makaazi

(3) Wizara ya Maji, Nishati na Madini

## WIZARA YA UJENZI, MAWASILIANO NA UCHUKUZI

***Mheshimiwa Spika,*** Ripoti yetu imeanza kwa kuichambua Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi, ambapo kwa hakika Kamati inaendelea kuipongeza Serikali kupitia Wizara hii kwa jitihada zake za kuhakikisha Miundombinu ya Usafirishaji pamoja na huduma za usafiri zinaendelea kuimarika siku hadi siku, hapa nchini.

***Mheshimiwa Spika,*** Pamoja na jitihada hizo, bado Wizara inapaswa

kuongeza bidii ya usimamizi na Utendaji hasa katika Miradi mikubwa ya Kimkakati ili kwenda sambamba na kasi ya Serikali ya Awamu ya Nane ya kuwaletea maendeleo wananchi. Kamati imechambua miradi Kadhaa ya Maendeleo inayotekelezwa na Wizara hii ikiwemo hii ifuatayo; -

**Mradi wa Ujenzi wa Barabara za ndani Unguja na Pemba**

***Mheshimiwa Spika,*** Miongoni mwa miradi iliyopewa kipaombele kikubwa na Kamati ni Mradi wa Ujenzi wa Barabara za ndani zenye jumla ya kilomita 275.9 Unguja na Pemba. Kamati imeshuhudia shughuli mbali mbali za utekelezaji wa mradi huu zikiendelea nchini kote ikiwemo usanifu, usafishaji na uwekaji wa kifusi na lami pamoja na ulipaji wa fidia za nyumba na vipando vilivyoathirika na ujenzi huo.

Kwa upande wa Pemba, Kamati ilikagua Ujenzi wa barabara ya Micheweni - Kiuyu - Mbuyuni Maziwangombe, na barabara ya Mapofu - Tumbe Kojifa - Bandarini. Kamati ilishuhudia kazi za ujenzi zikiwa zinaendelea vizuri ingawa tumebaini baadhi ya changamoto kama ifuatavyo: -

a) Kuna kila dalili za kutuwama kwa maji baada ya Ujenzi wa Barabara hizo unaondelea hivi sasa.

b) Nyumba nyingi katika maeneo ya mradi zimejengwa kwa

udongo, hivyo kuna hofu ya kuanguka endapo maji yanayotuwama hayatofanyiwa mpango wa kuhamishwa.

c) Kishindo cha Magari makubwa na zana za kazi kinaweza kuleta athari na uharibifu wa nyumba ambazo zipo karibu mno na barabara katika maeneo ya mradi.

***Hivyo basi,* Kamati** tunaishauri Wizara ihakikishe inafanya tathmini ya awali na yenye kujitosheleza kabla ya kuteua maeneo ya miradi ya barabara za ndani, ili kubaini athari zinazoweza kujitokeza wakati wa utekelezaji wa miradi hiyo. Aidha, Wizara ihakikishe inakuwa na mashirikiano ya kisekta ili kila taasisi iwe na njia za kupitisha miundombinu yake mapema na kuepusha uharibifu kwa kukata barabara muda mfupi tu baada ya ujenzi kukamilika.

**b) Ujenzi wa Barabara ya Chake - Wete**

Eneo jengine lililoanishwa katika Ripoti yetu na kuonekana na Changamoto kubwa ni **Mradi wa Ujenzi wa Barabara Kuu Nne Unguja na Pemba** hasa

Ujenzi wa **Barabara ya Wete – Chake** kilomita 22.1. Kamati imebaini hadi kufikia Disemba 31, 2023, shughuli hii imefikia asilimia 30% tu ya Utekelezaji. Kamati haikuridhika na hatua ya ujenzi iliyofikiwa, na inasikitishwa pamoja na kushangazwa na uvumilivu uliopo kwa wakandarasi ambao pamoja na kuaminiwa na Serikali bado hawaoneshi uwezo na utayari wa kufanyakazi kwa ubora na wakati uliopangwa.

## MAONI, USHAURI NA MAPENDEKEZO YA KAMATI

1) Kufuatia kasi ndogo ya ujenzi na visingizio vya kila siku na sababu za kila aina kwa mkandarasi wa barabara hii, Kamati inaiomba Serikali kufanya tathmini ya kina kuhusiana na uwezo wa Mkandarasi huyo.
2) Kamati inashauri sehemu ndogo inayokwisha kukamilika kwa kifusi iwekwe lami kama vile inavyoonekana katika barabara ya Kiembe Samaki – Amani ili kuepusha hasara inayoweza kujitokeza kwa kifusi hicho kukaaa muda mrefu na barabara kuanza kuchimbika kabla ya ujenzi wa lami kuanza.

### Suala la Ongezeko la Ajali na Utekelezaji wa Adbabu za papo kwa Papo

***Mheshimiwa Spika,*** Ripoti yetu pia inaizungumzia Mamlaka ya Usafiri na Usalama Barabarani ambayo miongoni mwa majukumu yake ni kupunguza ajali. Kamati inabainisha kwamba katika kipindi cha Julai - Disemba, 2023,

jumla ya ajali za barabarani **100** zimeripotiwa kutokea Unguja na Pemba, kati ya ajali hizo, vifo ni **103** na majeruhi **116**.

Aidha, jumla ya makosa **14,806** yenye thamani ya **TZS 323,716,500** yameripotiwa, kati ya makosa hayo makosa **9,331** yamelipiwa sawa TZS **215,723,900** na makosa **5,475** ni madeni sawa na TZS **107,992,600.**

### Changamoto za Mfumo wa Adhabu za Papo kwa Papo

Kamati imebaini kuwa, katika utekelezaji wa majukumu ya Mamlaka ya Usafiri wa Barabarani, Mamlaka hii inakabiliwa na changamoto kadhaa zinazopunguza ufanisi wa utendaji ikiwemo mfumo wa adhabu za papo kwa papo. Baadhi ya Changamoto hizo ni hizi zifuatazo: -

a) Kumaliza muda kwa nambari ya malipo (Control Number) ya adhabu za papo kwa papo kunakosababishwa na kucheleweshwa kwa malipo kwa muda uliowekwa.

b) Wananchi kuchelewa kufanya malipo ya adhabu kwa wakati kunakopelekea kurundikana kwa madeni, na

c) Mashine za POS kutumika kwa matumizi mengine kama vile kuweka game pamoja na azam TV katika vifaa hivyo.

**Hivyo, Mheshimiwa Spika,** Kamati inaishauri Wizara kupitia Mamlaka ifanye marekebisho juu ya namna bora ya utekelezaji wa mfumo wa

adhabu za papo kwa papo ili changamoto zilizojitokeza ikiwemo kumaliza muda kwa nambari ya malipo ziweze kurekebishwa.

Aidha, tunaiomba Mamlaka izidishe kasi ya Usimamizi wa Sheria, Kanuni na Miongozo ya Usalama barabarani ikiwemo waendesha bodaboda ili kupunguza ajali na vifo vinavyochangia kupunguza nguvu kazi ya taifa.

## Shirika la Bandari Zanzibar (ZPC)

***Mheshimiwa Spika,*** Kwa mara nyengine tena Kamati ya Mawasiliano, Ardhi na Nishati inaipongeza Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kupitia Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi chini ya Taasisi yake ya Shirika la Bandari kwa kufunga mkataba na Afrika Global Logistic (AGL). Kampuni hiyo inategemewa kuendesha Bandari ya Malindi kwa kipindi cha miaka mitano na imesajiliwa kwa jina la Zanzibar Multipurpose Terminal (ZMT).

Ripoti ya Kamati hii inabainisha mafanikio kadhaa yaliyopatikana baada ya Shirika la Bandari kukabidhiwa kwa Muendeshaji ikiwemo; -

1. Kuongezeka kwa Stahiki za wafanyakazi (Incentives) pamoja na mishahara yao;

2. Ulinzi na usalama umeimarika ikiwemo kuingia na kutoka kwa watu na vyombo vinavyoingia bandarini;
3. Kutumia mifumo ya teknolojia ya kisasa katika kutoa huduma za kiforodha.

**Madai ya Wadau baada ya Bandari ya Malindi Kupewa Muekezaji**

***Mheshimiwa Spika**,* Kamati ilifanya vikao tofauti na Viongozi wa Shirika la Bandari, Wadau wa Bandari pamoja na Uongozi wa ZMT, katika vikao hivyo, wadau walitoa changamoto kadhaa ikiwemo hizi zifuatazo: -

a) Ufanisi Mdogo Katika Utoaji wa Huduma kwa Meli za Makasha "container".

b) Kuengezeka kwa Tozo za Bandari kwa Wadau wa Majahazi na Meli za Ndani.

c) Kubadilika Utaratibu wa Malipo na Utoaji wa Huduma kwa Meli za Ndani (Local Vessel).

d) Kuchelewa Kutoka kwa Mizigo ya Wateja Baada ya Kukamilisha Hatua za Malipo.

***Mheshimiwa Spika,*** Kamati imebani kwamba madai yote hayo ya Wadau kwa kiasi kikubwa Serikali imefanya juhudi mbali mbali za kuyasawazisha. Hivyo, Kamati inaiomba Wizara kupitia taasisi yake ya Bandari kuzidi kutoa taaluma na ufafanuzi kwa wadau na wananchi kwa ujumla ikiwemo mpango wa elimu kwa Umma kama zilivyofafanuliwa kwa kina ndani ya ripoti yetu.

**Sehemu za Ukaguzi wa Abiria na Mizigo Bandarini na Viwanja vya Ndege**

***Mheshimiwa Spika***, Ripoti pia imegusia suala la malalamiko ya matumizi mabaya, pamoja na kuvunjiwa heshima kwa baadhi ya abiria hasa viongozi katika sehemu za upekuzi wa abiria na mizigo kwa abiria wa kawaida pamoja na ile ya Watu mashuhuri (VIP) ndani ya Bandari ya Zanzibar, Bandari ya Mkoani, Uwanja wa Ndege Zanzibar pamoja na Uwanja wa Ndege Pemba.

Hivyo, Kamati inaishauri Wizara kuwa na utaratibu mzuri wa mafunzo kwa wafanyakazi wake hasa mafunzo ya Huduma kwa Wateja (**Customer Care**) kwa watendaji wanaotoa huduma moja kwa moja kwa wananchi katika sehemu hizo. Aidha, Wizara iweke utaratibu maalum utakaozingatia matumizi sahihi ya eneo la watu mashuhuri (VIP) Bandarini na Viwanja vya

Ndege.

***Mheshimiwa Spika,*** Kamati pia imechambua Changamoto za Wakala wa Barabara Zanzibar ambayo inakabiliwa na Uchakavu pamoja na Uwepo wa Mashimo katika njia nyingi Unguja na Pemba, Uvamizi wa Maeneo ya Hifadhi ya Barabara kwa Ujenzi holela, pamoja na Wizi na Uharibifu wa Alama za Barabarani. Kufuatia changamoto hizo, Kamati inaiomba Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji kuchukua hatua zifuatazo: -

1) Wakala wa Barabara ifanye jitihada za kutafuta suluhisho la kudumu la kudhibiti kuchimbika ovyo kwa barabara zetu na kuondosha adha ya barabarani hasa wakati wa mvua.

2) Wizara ifanye mazungumzo na taasisi mbali mbali ili kuweza kusaidiana katika kusimamia utekelezaji wa sheria zilizopo na kuweza kudhibiti changamoto ya uvamizi wa hifadhi ya barabara kwa shughuli za ujenzi na biashara.

3) Wizara iendelee kuchukua hatua za kutoa taaluma kwa jamii juu ya umuhimu wa uwepo na matumizi ya alama za barabarani na hasara inayopatikana kwa jamii na Serikali iwapo vitendo vya wizi na uharibifu wa alama hizo

vitaendelea.

***Mheshimiwa Spika,*** Tukiiangalia Ripoti yetu katika kipengele kinachohusu Mamlaka ya Usafiri Baharini (ZMA) tunachambua hatua ya kuimarika kwa Usafiri wa majini hapa nchini. Kamati ilisafiri na Boti ya *Zanzibar 3,* inayomilikiwa na Kampuni ya Zanzibar First Ferries inayofanya safari zake kutoka Unguja/Pemba na Tanga. Kamati ilishuhudia uimara wa boti hiyo inayokwenda kwa kasi ambayo imesaidia kwa kiasi kikubwa kupunguza changamoto ya usafiri wa majini kwa wananchi wa Unguja, Pemba na Tanga.

**Mheshimiwa Spika,** pamoja na ahadi ya Serikali ya kutafuta Usafiri wa Umma wa Majini, Kamati inaishauri Wizara kuendelea kuweka mazingira mazuri ili kuwavutia wawekezaji kuleta vyombo vya kisasa vitakavyosaidia kutoa huduma za usafiri wa majini kwa wananchi wa Unguja, Pemba na Tanga.

***Vile vile Mheshimiwa Spika,*** Kamati inaitaka Mamlaka ihakikishe vyombo vyote vya majini vinavyopakia abiria vinatoa matangazo na kuwatambua abiria wote wenye mahitaji maalum kabla ya safari kwa ajili ya kuwawekea uangalizi maalum ikiwa ni miongoni mwa tahadhari ya kujikinga na maafa yanayoweza kujitokeza.

***Mheshimiwa Spika,*** kwa Upande wa Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji, Uwasilishaji wangu unamalizia na Wakala wa Majengo (ZBA) ambae anaendelea kukumbwa na Changamoto ya kukabidhiwa nyumba za Serikali ambazo ni chakavu zinazohitaji matengenezo makubwa, pamoja na uwepo wa wimbi la Miradi ya Serikali ambayo bado inaendelea kutekelezwa bila ya kupitia kwa Wakala wa Majengo Serikalini.

Kamati inaendelea kutoa wito kwa Serikali kuwatumia Wakala wa Majengo katika miradi yao ili waweze kutoa ushauri wa kiutaalamu na kuweza kusaidia kufanikiwa kwa miradi hiyo kwa ubora zaidi.

## WIZARA YA ARDHI NA MAENDELEO YA MAKAAZI

***Mheshimiwa Spika,*** Ripoti pia imechambua muundo na utendaji wa Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makaazi ambayo inadhamana ya kuhakikisha wananchi wanapata makaazi bora, salama na nafuu.

### Kamisheni ya Ardhi

***Mheshimiwa Spika*****,** Kuendelea kuwepo kwa Ardhi kubwa ambayo bado haijafanyiwa utambuzi na kusajiliwa kulingana na malengo ya usajili, pamoja na uvamizi wa maeneo kwa matumizi tofauti na yale yaliyoainishwa katika mipango mikuu ya matumizi ya ardhi ni miongoni mwa kasoro kubwa inayoleta Changamoto Katika Utendaji wa Kamisheni

ya Ardhi Zanzibar.

**Kadhalika,** Uvamizi katika maeneo ya wazi (open spaces), hifadhi ya barabara (Road reserve), viwanja vya michezo na fukwe, pamoja na Ukosefu mkubwa wa Mipango Miji na Vijiji, na ujenzi holela ni changamoto nyengine ya ugumu wa kupeleka huduma za kijamii ikiwemo barabara, mifumo ya maji safi, maji machafu na zimamoto.

***Hivyo, Mheshimiwa Spika,*** Kamati inaitaka Idara ya Mipango Miji na Vijiji kupitia Kamisheni ya Ardhi kuendelea na zoezi la upimaji ardhi katika maeneo tofauti mbali na yale ya Kilimo kwa Pemba na Uwekezaji Unguja.

Kamati pia inashauri utaratibu ulioanzishwa wa uwekaji wa Miji Mipya uende sambamba na ushirikishwaji wa taasisi zote zinazohusika na uwekaji wa miundombinu ili huduma za kijamii zifikishwe mapema na kwa uharaka katika maeneo husika kwa ajili ya kuepusha usumbufu wa kimiundombinu na kimazingira unaoweza kujitokeza hapo baadae.

***Mheshimiwa Spika,*** Katika kipengele cha Mahakama ya Ardhi Kamati inasisitiza kwa baadhi ya viongozi kuacha tabia ya kuingilia kesi pale ambapo zikiwa Mahkamani au tayari zimeshatolewa maamuzi, kwani

kufanya hivyo ni kuingilia uhuru wa Mahkama ambapo ni kosa kisheria, na wakati mwegine husababisha kuibuka kwa migogoro mingine mipya katika jamii. Aidha, Kamati inasisitiza kwa Watendaji wa Masuala ya Ardhi kuwa wasimamizi wazuri na kamwe wasiwe chanzo cha Migogoro kwa kufuata ipasavyo Sheria, Kanuni na Miongozo iliyopo.

***Mheshimiwa Spika,*** Kwenye Sekta ya Ardhi Ripoti pia imegusia masuala ya Ofisi ya Mthamini Mkuu wa Serikali ambayo ni dhamana katika usimamizi mzuri wa uthaminishaji rasilimali kwa malengo mbali mbali ya Sekta ya Umma, Biashara na Wananchi kwa ujumla. Kamati ya Mawasiliano, Ardhi na Nishati imebaini changamoto kadhaa zinazoviza utendaji wa Afisi hiyo ikiwemo; - Uhaba wa Wataalamu wa fani ya Uthamini, Uhaba wa vyombo vya usafiri pamoja na Kukosekana kwa mfumo wa kisasa (kidigitali) wa kuhifadhia taarifa na ripoti za uthamini zinazofanywa na Ofisi.

**Mheshimiwa Spika,** licha ya Changamoto hizo bado Kamati inaihimiza Ofisi ya Mthamini Mkuu wa Serikali kutekeleza majukumu yao ipasavyo na waadilifu ili kupunguza lawama kwa wananchi wasioridhika na tathmini ya maeneo yao.

**Sekta ya Makaazi**

***Mheshimiwa Spika,*** Kamati inaendelea kuipongeza Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makaazi kupitia Shirika la Nyumba kwa jitihada zake za kuwapatia wananchi makaazi bora na endelevu kupitia miradi mbali mbali inayoitekeleza ikiwemo; -

a) Ujenzi wa majengo manne yenye nyumba 72 za Makaazi na maeneo ya biashara Mombasa - Kwa Mchina, na

**b)** Utayarishaji wa mradi wa nyumba za makaazi Nyamanzi, mradi wa nyumba za makaazi na biashara Kisakasaka kwa Unguja na mradi wa nyumba za makaazi na biashara Mfikiwa, Chake chake Pemba.

**Ukaguzi wa Kamati katika Miradi ya Shirika la Nyumba Pemba**

- **Ofisi za Shirika Micheweni Pemba na**
- **Matengenezo ya Nyumba ya Maendeleo Mtemani**

***Mheshimiwa Spika,*** Kamati ilishtushwa na taarifa za Shirika la nyumba ambapo lilitumia Jumla ya shilingi **21,378,000** kwa ajili ya Ukarabati wa Ofisi ya Shirika Micheweni pamoja na Shilingi **121,468,100** kwa ajili ya Matengenezo ya Nyumba za Maendeleo Mtemani Wete. Kamati

ilitembelea Miradi hiyo kwa vipindi viwili mfululizo kwa nia ya kujiridhisha juu ya shughuli hizo zilizotumia kiasi hicho cha fedha. Uchuguzi wa Kamati umebaini kwamba Ukarabati uliofanyika haulingani kabisa na thamani ya fedha iliyotumika.

***Mheshimiwa Spika,*** Kamati haikuridhika na Matumizi ya fedha hizo pamoja na kazi iliyofanyika katika miradi hiyo na inawashauri sana Shirika la Nyumba kuwa waadilifu katika matumizi na usimamizi wa miradi yao.

## WIZARA YA MAJI, NISHATI NA MADINI

***Mheshimiwa Spika***, kwa Upande wa Wizara ya Maji, Nishati na Madini yenye dhamana ya kutoa huduma nafuu, endelevu na zilizo bora kwa wananchi wote, Kamati ya Mawasiliano, Ardhi na Nishati inaunga Mkono mapendekezo ya kikao cha pamoja kati ya Idara ya Maendeleo ya Maji pamoja na Taasisi ya Afisi ya Rais Ufuatiliaji na Usimamizi wa Utendaji Serikalini (PDB) kilichofanyika mwezi wa Julai 2023, na namna ya kuondoa changamoto za upatikanaji wa maji safi na salama kwa maeneo ya Unguja na Pemba.

***Mheshimiwa Spika,*** Ripoti imeweka bayana mapendekezo mbali mbali

yatakayosaidia kufikia malengo ya Serikali ya kuhakikisha kuwa asilimia 95 ya wananchi wote wa Zanzibar wanapata maji safi na salama ifikapo mwaka 2025 ikiwemo; -

a) Kuimarisha mfumo jumuishi wa usimamizi wa huduma za usambazaji wa maji safi na salama

b) Kuongeza kasi katika kushughulikia tatizo la upotevu wa maji kabla ya kuwafikia walengwa.

c) Tathmini ya mageuzi ya uendeshaji wa ZAWA kwa lengo la kuimarisha ufanisi wa kiuendeshaji katika utowaji wa huduma, uendeshaji kibiashara pamoja na kuziimarisha ofisi za maji za Wilaya kwa kuzipa uwezo wa kujitegemea na kujiendesha wenyewe.

***Mheshimiwa Spika,*** Kamati inaipongeza Wizara ya Maji, Nishati na Madini kupitia Mamlaka ya Maji Zanzibar (ZAWA) kwa kutekeleza Miradi mbali mbali inayolenga kuimarisha huduma endelevu ya upatikanaji wa maji safi na salama kwa wananchi wote wa Zanzibar ikiwemo Uchimbaji wa visima, Ujenzi wa matangi ya kuhifadhia maji na Ulazaji wa mabomba kupitia Mradi wa Uhuishaji na Uimarishaji wa Mfumo wa Usambazaji Maji Zanzibar na Mradi wa Uimarishaji wa Usambazaji Maji Zanzibar kupitia fedha za ahueni

ya Uchumi na Ustawi wa Jamii UVIKO – 19.

## Hali Halisi ya Uzalishaji wa Maji

***Mheshimiwa Spika,*** Ripoti inabainisha kwamba hadi Disemba, 2023, hali ya uzalishaji maji imefikia wastani wa asilimia 70% kwa Unguja na Pemba, ambapo mahitaji ni lita **275,980,481** kwa siku, na uzalishaji ni lita **191,959,675** kwa siku, na mapungufu ni lita **84,020,806.** Aidha, ZAWA inaendelea kupambana na Upotevu wa maji hayo kabla ya kuwafikia walengwa ambapo jumla ya mivujo 882 imezibwa katika wilaya tofauti za Unguja na Pemba.

## Hali ya Madeni ya Wateja wa ZAWA

***Mheshimiwa Spika,*** Kamati imebaini kwamba hadi kufikia Disemba, 2023 ZAWA ilikuwa inadai jumla ya **TZS Bilioni 2,956,264,239.98** kutoka kwa wateja wake Unguja na Pemba, ingawa kwa bahati mbaya Mifumo ya ZAWA inashindwa kupambanua viwango vya madeni kulingana na makundi tofauti ya wateja wa maji ambayo ni: -

a) Wateja wa majumbani
b) Watumiaji wa Biashara
c) Wateja wa Taasisi na
d) Wateja wa Kilimo

***Mheshimiwa Spika,*** Kamati inaendelea kuisisitiza ZAWA kuwafuatilia wadaiwa wake wote na kuweka mikakati ya kuhakikisha kwamba wateja wao wanasawazisha madeni hayo. Aidha, Kamati inaitaka ZAWA kuweka Mifumo Imara ambayo inaweza Kuchanganua Madeni ya Wateja wake kulingana na Makundi yaliyopo.

***Mheshimiwa Spika*,** Maelezo kamili ya Utendaji wa ZAWA, mafanikio na Changamoto pamoja na ushauri wa Kamati umefafanuliwa kwa kina ndani ya Ripoti yetu ambayo kila mmoja wetu anayo katika vishkwambi vyetu.

**Idara ya Nishati na Madini**

***Mheshimiwa Spika,*** bado Kamati inaendelea kusononeshwa na athari zinazojitokeza katika Maeneo ya Uegeshaji wa gari zinazosafirisha Maliasili zisizorejesheka. Ripoti imebainisha Changamoto zilizoibuliwa na Kamati katika maeneo hayo kama zifuatazo: -

a) Kuendelea kwa vitendo vya uchimbaji holela wa mchanga katika maeneo yasiyo rasmi hali ambayo inaharibu mazingira pamoja na ukosefu wa mapato ya Serikali;

b) Kuvamiwa kwa maeneo ya hifadhi ya njia kuu ya umeme itokayo Fumba kuelekea Meli Nne TAVETA;

c) Uchafuzi wa mazingira unaoweza kupelekea maradhi ya mripuko ikiwemo malaria na kipindpindu;

d) Vitendo vya utumiaji wa madawa ya kulevya ikiwemo bangi ambavyo vinaweza kuhatarisha ustawi kwa jamii wa maeneo ya karibu na sehemu ya maegesho.

***Mheshimiwa Spika*,** Kufuatia changamoto hizo Kamati inaiomba Wizara kuendelea kutafuta maeneo maalum ya maegesho ya gari zinazotoa huduma ya usafirishaji wa Maliasili zisizorejesheka kwa wananchi wenye mahitaji madogo.

**Shirika la Umeme Zanzibar (ZECO)**

***Mheshimiwa Spika,*** Hali ya Miundombinu ya Umeme Unguja na Pemba inaonesha kwamba Uwezo wa Waya wa laini kubwa uko ukingoni, kutokana na kuyoyoma kwa kiwango cha Megawati zilizokusudiwa. Hali hii tumebaini inasababishwa na ukuaji wa shughuli za kiuchumi ndani ya visiwa vya Zanzibar kunakokwenda sambamba na mahitaji ya matumizi ya umeme hapa nchini, ambapo mahitaji ya juu yamefikia Megawati 112.13 sawa na asilimia 77.33% kwa waya zote mbili zilizopo.

Aidha, Kamati imebaini kwamba upande wa Pemba mahitaji ya juu ya

umeme yamefikia megawati 13.16 sawa na asilimia 65.8 ya uwezo wa waya unaotumika hadi sasa wa Megawati 20.

***Mheshimiwa Spika,*** Ripoti pia inabainisha changamoto kadhaa za **ZECO** ikiwemo Uharibifu wa Miundombinu ya Usambazaji wa Umeme na wizi wa Nyaya za shaba. Kamati inalitaka Shirika liongeze bidii ya utoaji wa elimu kwa umma juu ya madhara na athari zinazotokana na uvamizi, wizi na uharibifu wa miundombinu ya umeme.

Aidha, Kamati inashauri na kusisitiza nguzo zinazobadilishwa ziwe zenye viwango na uimara zitakazopelekea kudumu kwa muda mrefu na pia kuanza kufikiria kupitisha Umeme chini ya Ardhi kwa kutumia waya Maalum (Amal Cable).

**Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Maji na Nishati (ZURA)**

***Mheshimiwa Spika*****,** Kamati inamalizia Ripoti yake kwa kuwasilisha Shughuli za Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Maji na Nishati Zanzibar – ZURA ambayo imeonekana kutanua Wigo zaidi wa Udhibiti wa Huduma za Maji na Nishati. Changamoto zilizobainika katika ukaguzi wa miundombinu na mazingira ya vituo vya uzalishaji maji ni pamoja na: -

a) Visima kukosa uzio ambao unatoa uhifadhi mzuri wa vyanzo hivyo.

b) Uwepo wa mivujo na upotevu wa maji katika baadhi ya miundombinu ya maji.

c) Kukosekana vifaa vya dharura wakati wa hatari katika vituo vyote.

d) Kukosekana pampu za dharura (standby pump).

***Mheshimiwa Spika,*** Ripoti pia imechambua Kasoro kadhaa Zilizobainika Kupitia Ukaguzi wa ZURA Katika Maeneo ya ZECO ikiwemo Transforma katika sehemu za kupokelea umeme mkubwa (High Voltage) zimeungwa moja kwa moja kwa kutumia waya (fuse element).

Kamati inaishauri ZURA kuchukua hatua kwa kuitaka ZECO na ZAWA kufanya marekebisho ya kasoro zilizojitokeza pamoja na kuzingatia taratibu za kiusalama na ubora wa huduma za umeme na maji yanayosambazwa kwa wananchi.

***Mheshimiwa Spika,*** Kamati ya Mawasiliano, Ardhi na Nishati ya Baraza la Wawakilishi inakamilisha Ripoti yake ya Mwaka 2023/2024 kwa kuwapongeza kwa dhati Mawaziri, Manaibu Mawaziri, Makatibu Wakuu, Manaibu Katibu Wakuu pamoja Viongozi na watendaji wote kwa Ujumla wa Wizara zote tatu zinazosimamiwa na Kamati hii kwa mashirikiano makubwa waliyoipatia Kamati kwa kipindi chote cha utekelezaji wa majukumu yake ya Kikatiba na Kikanuni.

Aidha, kwa umuhimu mkubwa Kamati inakupongeza kwa dhati wewe binafsi Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Naibu Spika, Wenyeviti wa Baraza, Katibu wa Baraza la Wawakilishi, pamoja na sekretariati yote ya Baraza la Wawakilishi kwa kuiwezesha vyema Kamati kutekeleza majukumu yake na kuweza kutayarisha ripoti yake kwa mwaka 2023/2024.

Kamati inashauri mashirikiano hayo yaendelezwe kwa kipindi chote kinachofuata ili kuweza kufikia malengo yaliyokusudiwa.


***Mheshimiwa Spika,*** Kipekee Naomba kutumia nafasi hii tena kuwashukuru Wajumbe wa Kamati hii, kwa mashirikiano yao makubwa ambayo yameiwezesha Kamati kufanyakazi kwa ufanisi na uweledi mkubwa. Kwa ruhusa yako sasa naomba niwatambue Waheshimiwa Wajumbe hao pamoja na Makatibu wa Kamati kama ifuatavyo: -

| Nam | JINA | WADHIFA |
|---|---|---|
| 1. | Mhe. Yahya Rashid Abdalla | Mwenyekiti |
| 2. | Mhe.  Aza Januari Joseph | Makamu Mwenyekiti |
| 3. | Mhe. Ameir Abdallah Ameir | Mjumbe |
| 4. | Mhe. Issa Haji Ussi (Gavu) | Mjumbe |
| 5. | Mhe. Hassan Hamad Omar | Mjumbe |
| 6. | Mhe. Hudhaima Mbarak Tahir | Mjumbe |
| 7. | Mhe. Mwanajuma Kassim Makame | Mjumbe |

| | | |
|---|---|---|
| 8. | Mhe. Fatma Ramadhan Mohammed | Mjumbe |
| 9. | Ndg. Himid Haji Choko | Katibu |
| 10. | Ndg. Salma Muhsin Haji | Katibu |
| 11. | Ndg. Saad Othman Saad | Katibu |

***Mheshimiwa Spika,*** Mwisho nawaomba waheshimiwa wajumbe kuisoma, kuichangia na hatimae kuikubali ripoti yetu ili hatimae kuongeza uwajibikaji na ufanisi bora na wenye tija katika nchi yetu. Ahsanteni sana kwa kuniskiliza.

***Mheshimiwa Spika*,** Naomba kutoa hoja.



…………………………….

**Mheshimiwa Yahya Rashid Abdulla,**
**Mwenyekiti,**
**Kamati ya Mawasiliano, Ardhi na Nishati,**
**Baraza la Wawakilishi,**
**ZANZIBAR.**